# *Kuweka Wakfu*

Mungu akubariki, ndugu.

2 Habari za asubuhi kwa wote. Kweli ni majaliwa kuwa hapa asubuhi ya leo katika kanisa hili dogo la kupendeza, kwa ajili ya ibada ya kuweka wakfu tena. Kama nilivyokuwa tu nikizungumza na Dada Hoover kwenye chumba cha nyuma, alisema wakati mmoja lilikuwa, ninaamini, kanisa la Pilgrim Holiness ama la United Brethren. Pilgrim Holiness, ninaamini. Naam. Na sasa linawekwa wakfu tena kwa ajili ya full Gospel, na hii ni ibada ya kuweka wakfu tena.

3 Na mchungaji wake mzuri, kama sote tujuavyo, Ndugu Hoover ni mvulana mwaminifu sana, aliyejitolea.

4 Mama yake, nilimfahamu, miaka kadhaa iliyopita, yeye na familia yangu walikuwa tu ni kama . . . Watoto, hata wanamwita, "Mammy Hoover," kwa sababu kwamba kidogo yeye . . . Alikaa pamoja nasi kwa muda mrefu wakati watoto walipokuwa wachanga, na—nao wanamfahamu tu jinsi hiyo, mama mzee mtauwa, mtakatifu.

5 Na mvulana wake mhubiri mzuri ambaye aliomba sana kwa ajili yake, ameyatoa maisha yake kwa Kristo, na kuweka wakfu maisha yake kwa ajili ya utumishi wa Mwenyezi Mungu. Na sasa, leo hii, amesimama, akilichukua kanisa, ama hili jengo hapa, ambapo labda limekaa bila kutumika kwa muda mrefu, apate kuiendeleza Injili, kwa namna ya Injili yote, kipimo.

6 Bibi Hoover alikuwa tu akiniambia, Bibi L. G. Hoover, alikuwa tu akiniambia huyo alikuwa ni msichana wake mdogo akiupiga ule wimbo, dakika chache zilizopita, ule wimbo wa kuja wa *Amini Tu,* naye ni mpiga piano hapa kwenye—kwenye piano. Miezi mitatu iliyopita, wakati walipoingia, wao . . . asingeweza kupiga tuni yoyote. Lakini sasa anaweza kupiga. Hilo ni zuri sana, sana.

7 Ninaye msichana anayeketi hapa nyuma, ambaye amekuwa akifanya masomo ya muziki kwa yapata miaka mitano, ama zaidi, nami sijui ilivyonigharimu, na piano mpya. Asingeweza kucheza wimbo vizuri kama maskini mtoto yule alivyokuwa akiucheza. Kwa hiyo inaonyesha jinsi vipaji vilivyotolewa na Mungu vilivyo, na halafu jambo fulani unalojaribu kujibunia. Mnaona?

8 Sasa, tunashukuru kwamba Mungu amewapa watu hawa mahali hapa. Nami ninatumaini ya kwamba patakuwa ni mnara mkuu wa taa kwa ajili ya sehemu hii ya nchi.

9 Sasa, mara nyingi watu wanadhani kwamba wanapoliona kusanyiko . . . Basi wanawazia, "Vema, maskini kanisa hili dogo

halitaenea watu wengi sana." Na—nami ninaamini Ndugu L. G. aliniambia, ama njia fulani, kwamba kusanyiko lake lilikuwa na kadiri ya watu sabini ama themanini, na kitu kama hicho. Huenda niko chini kidogo ama juu kidogo, lakini ni karibu hapo, ndio kwanza tu lianze.

10 Wangewazia, "Vema, angalia makanisa katika ninii . . . kote nchini leo hii, ambayo makusanyiko yao yanafikia kiwango cha maelfu." Na labda, mengine, kwamba kila siku ya ibada wana maelfu.

11 Lakini, kulitia moyo kundi hili dogo, hiyo siyo hasa ambayo Mungu anaangalia, idadi. Yeye—Yeye huangalia . . . Yeye daima hajiweki juu ya msingi wa wingi, bali katika ubora. Mnaona?

12 Tunaona katika Biblia katika mlango wa 19 wa Matendo, ambapo, "Paulo, akipitia kati ya nchi za juu alifika Efeso, na huko akapata kanisa." Hilo lilikuwa ni kanisa la Efeso, ambalo lilikuwa ndilo la kwanza katika wakati wa kanisa, uliozingatiwa katika Ufunuo wa Kristo. Na katika kanisa hili hapa, kulikuwako na watu kumi na wawili, kama ilivyorekodiwa. Idadi yake ilikuwa ni watu kumi na wawili.

13 Lakini kama kanisa hili lilikuwa tu na watu kumi na wawili, ama kama lile kanisa lilivyokuwa, nao wamejitolea kabisa kwa Mungu, Yeye anaweza kufanya mengi zaidi na hao kumi na wawili kuliko anavyoweza kufanya na ulimwengu wote. Ni kule kujitolea tuliko nako. Ambako Kweli ya Injili, sio tu kwamba inatoka jukwaani, bali inapata pumziko lake mioyoni mwa watu na kutenda kazi. Kwa hiyo ninahesabu hii kwamba ni furaha asubuhi ya leo.

14 Nilipofika mlangoni, nilimsikia Ndugu Beeler akifanya maombi, nami nilikuwa nikimwazia kwamba ni askari mstaafu, na hii ikiwa ni Siku ya Kukomesha Vita. Na, hakika, sote tuna furaha kwamba kulikuwako na Siku ya Kukomesha Vita. Na kunaweza pia kuwa na si—siku ya kukomesha vita hapa kanisani, ambapo watu ambao wamekuwa vitani pamoja na nafsi zao, dhidi ya Mungu, wanaweza kutia sahihi siku ya kukomesha vita leo, wawe na amani na Mungu kupitia Yesu Kristo. Ninaamini Warumi 5:1 ilisema, "Basi tukiisha kuhesabiwa haki kwa imani, tunayo amani na Mungu kwa njia ya Bwana wetu Yesu Kristo."

15 Na sasa nimeona baadhi ya watu walioketi hapa, Ndugu na Dada Bryant, na baadhi ya marafiki hapa kutoka maskanini. Sasa, asubuhi ya leo, nilikuwa nizungumze juu ya somo la shule ya Jumapili asubuhi ya leo maskanini, bali nimeliahirisha mpaka usiku wa leo, kwa sababu ya kuja hapa kwa ajili ya huku kuweka wakfu. Ibada zitaanza mapema usiku wa leo, mnaona, huko maskanini. Ninakusudia kuwa jukwaani, nikiwa tayari kuanza kuzungumza saa moja, kusudi tusichelewe. Nami ninao u—ujumbe mrefu. Somo ni: *Kwa Nini Nimekuwa Nikipinga*

*Dini Ya Kimadhehebu.* Nalo limefundishwa katika Maandiko. Kwa hiyo, ninyi jamaa maskanini, mlio huko, vema, ninyi njoni mapema.

16 Sasa, Ndugu Hoover, si—sijui jinsi ya kumshukuru Bwana, asubuhi ya leo, kwa ajili ya kijana mwanamume ambaye amejitolea kwa Kristo, na miongoni mwa watu wake hapa, kuuleta ujumbe huu adhimu wa Kristo kwa watu hawa. Mimi mwenyewe, ni Mkentaki. Nimetoka tu huku chini barabarani mbali kidogo, kutoka kwenye mji mdogo unaoitwa Burkesville. Na mimi. . .ninawaomba ninyi watu hapa karibu, kama Mkentaki mmoja kwa mwenziwe, njoni mkamsikilize mvulana huyu. Tokeni miongoni mwa watu hapa, mkasambaze habari kila mahali, na mwingie. Muwaingize ndani. Ikibidi, Biblia ilisema, muwaamrishe, muwashurutishe kuingia. "Enendeni kwenye barabara kuu na mipakani m—mkawashurutishe," hiyo ni kuwalazimisha, "kuingia ndani."

17 Naye Ndugu Hoover, nimemfahamu kwa miaka michache sasa. Nami ninamjua kuwa ni mvulana mtauwa, aliyejiweka wakfu. Bwana daima na azibariki jitihada zake. Niliisikia maskini kwaya yenu. Ni—nilijaribu kuangalia mlangoni, ndi—ndipo nikaisikia maskini kwaya hiyo ikiimba, "Iweni na hakika kabisa." Hiyo ni kweli.

18 Unaweza ukawa shaghalabaghala kuhusu kitu chochote kingine, bali inapofikia kwenye kikomo chako cha Milele, afadhali uwe na hakika kabisa. Unaona? Liweke tu hilo niani mwako, "Kuwa na hakika kabisa, kabisa." Usibahatishe juu ya hilo. Kama ulienda kwenye mkahawa, ukaagiza bakuli ya supu, na kwenye hiyo supu mlikuwamo na buibui mkubwa, hakika ungeisukumia mbali. Kamwe usingeigusa, la, bwana, kwa sababu labda ingekuua. Ile sumu ya buibui huyu, iliyopikwa kwenye supu hii, huenda ikasababisha kifo chako. Kwa hiyo ikiwa wewe ni mwangalifu sana kuhusu mwili huu, ambao hauna budi kufa, mnaona, vipi kuhusu ile nafsi ambayo si lazima ife?

19 Kwa hiyo ninapenda Neno lote la Mungu katika mfano wa Injili yote. Na kwa hiyo ninajua na ninaamini, na ninayo matumaini, ya kwamba Ndugu Hoover ataitimiza ahadi yake kwa Mungu, kuihubiri Hiyo vizuri sana ajuavyo, Injili yote.

20 Akiketi pale, akimsikia maskini mpiga piano akipiga sauti hiyo, *Amini Tu.* Mwanangu, Billy Paul, sidhani yupo papa hapa, wakati huu. Lakini nilisema, "Billy, waisikia maskini sauti hiyo ya piano ikipiga *Amini Tu*?" Nimeusikia wimbo huo mdogo katika karibu kila lugha chini ya Mbingu, ukiniita jukwaani, kutoka kwenye maeneo yaliyogandamana ya Aktiki mpaka kwenye misitu ya tropiki ya huko Kusini, chini ya ardhi, kote duniani. *Amini Tu,* katika kila namna za sauti, ukiniita jukwaani. Siku moja, wakati maisha yangu yatakapokwisha

duniani, ninatumaini watauimba huo wakati wakininii... nisipoishi kuona Kuja Kwake, wakati wakiniweka mbali. Ninamwamini Yesu Kristo.

21 Sasa, ninayo Maandiko fulani hapa, ambayo ningetaka kuyarejea, katika huku kuweka wakfu tena kwa jengo hili, yanayotoka kwenye Biblia. Nami ninafikiri ya kwamba, sasa, kwamba kanisa hili halijawekwa wakfu kwa ajili ya dhehebu. Limewekwa wakfu kwa utumishi wa Mungu.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa, tunapoomba.

22 Baba Mtakatifu na mwenye rehema, tunapokuja Uweponi Mwako, tukikiacha chumba hiki, kwa imani, tunakuja kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, ambako Madhabahu yale ya dhahabu yametandaa kutoka anga hata anga, ambako kila mwanadamu, kanuni ya imani, jamii, ama rangi ana haki ya kuja, kila kiumbe, ambacho Kristo alikifia na kujilaza Mwenyewe juu ya Madhabahu hayo, kama sadaka yetu kwa ajili ya dhambi. Tuna haki ya kuja kwa ujasiri kwenye Kiti cha rehema. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya majaliwa haya makuu ambayo tunaweza kuwa nayo leo hii, na tunayo. Tunakushukuru Wewe kwa ajili ya kila mshiriki wa Mwili Wako duniani leo hii, ambaye amekuja kwenye Kiti hiki kikuu cha Enzi, na amekubali sadaka ya amani, na amani ipitayo fahamu, ya Injili.

23 Sasa tunaomba, Mungu, kwa ajili ya kanisa hili, kundi hili la watu linalokuja kwenye maskini jengo hili asubuhi ya leo kwa ajili ya kujiweka wakfu kwa upendo, na ishara za mikono yao na moyo, kuandaa mahali ambapo watu wanaweza kuja, wakaabudu. Nasi tunaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utabariki jitihada zao. Pia tunaomba ya kwamba Wewe utambariki mchungaji, ndugu yetu mwenye fadhili, na mke wake, familia yake, mashemasi, wadhamini, halmashauri, washirika, na wote, pamoja.

24 Na sasa tunapolifungua Neno Lako, leo hii, kwa ajili ya faraja, kujua kama mambo haya tufanyayo yanaambatana na Maandiko, kwa kuwa wakati umeenda kuliko tunavyodhania. Tunajisikia, leo hii, ya kwamba hakuna wakati mwingi sana uliosalia. Lakini hatuna budi kuingia kazini. Hatuna budi kuwa tukisihi na kushurutisha, kwamba kila mshiriki ambaye amechaguliwa awali, kwa Mwili wa Kristo, kwamba tueneze Ujumbe huu mpaka kila mtu apate kusikia, mpaka tuwe na hakika kwamba kila jitihada ambayo tungaliweza kuweka imewekwa. Baba, libariki Neno Lako, na useme nasi sasa kupitia Neno Lako, wakati tukisikiliza kwa mioyo misikivu na masikio yaliyofunguliwa, kuyapokea kwa furaha yale Wewe ungetutaka tuyajue. Tunaomba hayo katika Jina la Yesu. Amina.

25 Sasa, huenda kukawa na wengi wenu, ambalo ni kawaida, kwamba watu wakati mwingine huyatia alama Maandiko, ama

kuyaandika, ama kuandika muhtasari. Nami hufanya vivyo hivyo. Na kama mkitaka kufungua pamoja nami sasa, kwa somo la kwanza la Maandiko, nina sehemu tatu ningetaka kusoma asubuhi ya leo. Na hapo ni, Mambo ya Nyakati ya Kwanza 17:1 hadi 2, na Matendo 7:44-49, na Waebrania 10:1. . . 5.

26 Sasa kwanza tutasoma kutoka Mambo ya Nyakati ya Kwanza 17, kuanzia kifungu cha kwanza. Halafu basi, pili, tutasoma katika Kitabu cha Matendo ya mitume, kwenye—kwenye mlango wa 7. Tungetaka kuanza kusoma kwenye kifungu cha 44 cha mlango wa 7 wa Matendo, yote yakihusu kuwekwa wakfu kwa hekalu. Na halafu Waebrania 10:5.

> *Ikawa, Daudi alipokuwa akikaa nyumbani mwake, Daudi akamwambia nabii Nathani, Angalia, mimi ninakaa katika nyumba ya* mwerezi, *bali sanduku la agano la* BWANA *linakaa chini ya mapazia.*
>
> *Naye* Nathani akamwambia *Daudi, Fanya yote yaliyomo moyoni* mwako*; kwa maana Mungu yu pamoja nawe.*
>
> *Ikawa usiku uo huo, neno la Mungu likamjia Nathani, kusema,*
>
> *Nenda. . .mwambie mtumishi wangu, Daudi,* BWANA *asema hivi, Wewe hutanijengea nyumba ya kukaa:*
>
> *Kwa maana sikukaa ndani ya nyumba tangu siku ile nilipowaleta Israeli huku, hata leo; lakini hema kwa hema nimehamia, na maskani kwa maskani.*

27 Sasa katika Kitabu cha Matendo ya mitume, kuanzia wa 7, na kifungu cha 44.

> *Baba zetu walikuwa na ile hema ya ushahidi huko jangwani, kama alivyoagiza yeye aliyesema na Musa, ya kwamba aifanye sawasawa na mfano ule aliouona.*
>
> *Ambayo pia baba zetu, kwa kupokezana, wakaingiza pamoja na Yesu katika milki ya Mataifa wale, ambao Mungu aliwafukuza mbele ya baba zetu, mpaka siku za Daudi;*
>
> *Aliyepata fadhili mbele za Mungu, naye* aliomba *ampatie Mungu wa Yakobo maskani.*
>
> *Lakini Sulemani alimjengea nyumba.*
>
> *Ila Yeye aliye juu hakai katika nyumba zilizofanywa kwa mikono; kama vile asemavyo nabii,*
>
> *Mbingu ni kiti changu cha enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu yangu: ni nyumba gani mtakayonijengea? asema Bwana: au ni mahali gani nitakapostarehe?*
>
> *Si* mikono *yangu iliyofanya haya yote?*

28 Na katika Kitabu cha Waebrania, mlango wa 10 na kifungu cha 5.

> *Kwa hiyo ajapo ulimwenguni,* alisema, *Dhabihu na* matoleo *hukutaka, lakini mwili umeniwekea tayari:*

29 Tuna uzoefu sana na usomwaji wa Maandiko haya tunayotaka kuyazungumzia kwa dakika chache.

30 Sasa, Daudi, chini ya shauku na ufunuo, aliwazia moyoni mwake, jambo zuri sana. Wakati, Daudi, akiwa ni mtu mwema, na aliyependwa sana na watu, naye Mungu alikuwa amembariki kwa njia nyingi sana. Basi akasema, "Sasa ni haki mimi kukaa hapa katika nyumba nzuri ambayo Bwana amenipa, nalo sanduku la agano la Mungu wangu liko huko nje chini ya mapazia?" Hilo lilikuwa ni jambo zuri sana. Ilikuwa ni ufunuo, kwa Daudi kujua jambo hili. Kwa sababu haikuwa ni haki kabisa kwake kuwa na mahali pa—pa kupendeza namna hiyo, chini ya nyumba iliyojengwa kwa mwerezi, ambapo palikuwa ni mahali pa gharama kubwa sana; ndipo akasema basi, "Sanduku la agano la Mungu wangu, Ambaye alinipa vitu hivi vyote, lingali huko nje chini ya mahema."

31 Naye Nathani, yule nabii, akijua ya kwamba Mungu alikuwa pamoja na Daudi, yeye alisema, "Daudi, fanya yote yaliyo moyoni mwako, kwa kuwa Mungu yu pamoja nawe." Vinginevyo, Mungu anapokupa ufunuo, utekeleze. Lakini hayo yote yalikuwa yakifanya kazi.

32 Basi usiku huo, Bwana akamjia mwonaji huyu, na nabii Nathani, akasema, "Nenda, kamwambie mtumishi wangu, Daudi." Mnaona? Ninapenda hilo. Loo, kwa maneno mengine, "Napenda ujasiri wake, na mawazo yake Kwangu, kunijengea Mimi mahali. Lakini," Yeye akasema, "Si—sijakaa katika nyumba. Sijakuwa na mahali pa kukaa ninaposhuka duniani, kuwaangalia watu Wangu. Sijakuwa na mahali pa kukaa, hata tangu nilipowaleta Israeli. Sijamwamuru yeyote wa waamuzi kunijengea nyumba ya mierezi, lakini nimehamia hema kwa hema." Hivyo si ni karibu jinsi ilivyo siku hizi! "Nimehamia hema kwa hema, na mahali mahali, kukutana na watu Wangu."

33 Akasema, "Nenda, kamwambie Daudi," kama Maandiko yanavyoendelea kusema, "Nalikutoa katika zizi lile la kondoo huko nje, ukiwaandama hao kondoo wachache wa baba yako. Nami nikakufanyia jina kama la hao wakuu waliomo duniani. Nimewakatilia mbali adui zako, kutoka mkono wa kulia hadi mkono wa kushoto. Ninakupenda, Daudi. Nami ninajua ya kwamba shauku zako ni za kweli. Ninajua kwamba shauku zako ni aminifu. Nami ninajua ya kwamba unanipenda."

34 Unaweza kuona Zaburi, jinsi ambavyo Daudi daima, anamwazia Mungu. Wengi wetu kupita kiasi siku hizi huwaza juu ya mafanikio yetu, jambo fulani ambalo tungeweza kufanya

kujiboresha wenyewe. Lakini Daudi daima alikuwa akiwazia yale angemfanyia Mungu.

35 "Ninajua shauku zako, Daudi. Nami ninataka ujue yale niliyokufanyia. Ulikuwa tu mvulana mdogo, asiyejulikana na mtu yeyote, na ninii yako . . . hata baba yako alikupatia kondoo wachache huko nje kuwachunga. Lakini nilikuwa pamoja nawe. Nami nimewakatilia mbali adui zako, kutoka mkono wako wa kulia hadi mkono wako wa kushoto. Lakini shauku zako ni sahihi. Lakini, Daudi, wewe ni mtu wa vita. Wewe ni mtu aliyemwaga damu. Siwezi kukuruhusu kufanya hili. Lakini nitakuahidi ya kwamba kupitia kwenye tunda la viuno vyako, nitamwinua mwana wako, naye atalijenga hekalu."

36 Sasa, sote tunajua ya kwamba ya duniani ni mfano tu wa ya Mbinguni. Ya kawaida ni mfano tu wa ya kiroho. Yule . . . Kweli, Yule aliyekuwa akizungumza habari Zake alikuwa ni Kristo, kwa ajili ya Hekalu.

37 Lakini yeye alikuwa ni Sulemani, mwana wa Daudi, katika mwili wa kawaida. Baadaye, tunasoma katika Wafalme wa Kwanza, kama ungetaka kulisoma, ya kwamba yeye—yeye alijenga maskani ambayo Daudi alitaka kujenga, kwa sababu Sulemani alikuwa ni mtu wa amani, wa hekima. Yeye hakwenda vitani, kama Daudi, na kumwaga damu nyingi. Yeye alikuwa tu ni mtu wa amani. Naye Mungu alimpa hekima. Wakati alipoulizwa alichotaka, mbele za Mungu, yeye aliomba tu apate hekima kujua jinsi ya kuwaongoza watu Wake. Wala kamwe hakuchukua karama kuu ambazo zingaliweza kufanywa, bali aliomba tu hekima apate kujua jinsi ya—ya kuwaongoza watu wa Mungu vizuri sana.

38 Nami nafikiri, sisi, katika kuomba, sisi wenyewe, laiti tungaliomba tu hilo, tupate tu ufahamu, kwa ajili ya jambo fulani ambalo litakuwa bora kwa ajili ya watoto wa Mungu. Kwa kweli nafikiri hilo ndilo wazo la mchungaji huyu la kulileta kanisa hili humu ndani, mnaona, kulichukua kanisa hili la kale na kuliweka wakfu tena leo. Anajaribu kupata mahali kutoka kwenye mvua, na theluji, na kadhalika, kwa ajili ya watu wa Mungu. Nafikiri Mungu angeliheshimu hilo katika mvulana huyu, kama tu vile alivyofanya katika Daudi.

39 Sasa, tunaona, kwamba pana matumizi makuu ya kiroho hapa, ambayo ningetaka hasa kuyarejea. Sasa, kama ukisoma Wafalme wa Kwanza, utaona ya kwamba, katika hili, Sulemani alianza, kama kijana, kulijenga hekalu hili ambalo baba yake alikuwa ameahidiwa, kupitia kwa Mungu, kwamba angelijenga. Mnaona, yeye anadumu moja kwa moja na Maandiko na ahadi. Sasa, hivyo ndivyo inavyotupasa kufanya sikuzote, tupate kufanikiwa, ni kudumu moja kwa moja na ahadi za Mungu. Haijalishi jinsi linavyoonekana ni jambo zuri sana kwenda *hivi*, ama *vile*, dumu pamoja na Maandiko. Naye Sulemani alijua

ya kwamba Mungu alikuwa amemwahidi baba yake, Daudi, ya kwamba yeye angelijenga hekalu.

40 Sasa, kama mkiangalia, nyenzo hazikupatikana Palestina pekee, kwamba, hekalu hili, maana hazikuwapo. Ilimbidi kwenda kote ulimwenguni, ulimwengu uliojulikana, kutafuta sehemu hizi ambazo zingeingia katika hekalu hili.

41 Hayo ni matumizi mazuri ya jinsi gani, kwamba Mungu hakati nyenzo zake kutoka kwa Wayahudi pekee, ama kutoka kwa wazungu pekee, ama kutoka kwa watu wa hudhurungi, ama wekundu, ama weusi, ama rangi yoyote wanayoweza kuwa, ama chochote kile, kutoka Marekani pekee, ama kutoka tu Canada, bali Yeye hukata nyenzo Zake kutoka kote ulimwenguni.

42 Na kama wakati walipokuwa wakikata jiwe la namna fulani lililopatikana katika sehemu kama hiyo ya nchi, na labda wakikata jiwe kwenye taifa jingine, lipate kuumana na jiwe hili lililokatwa katika ninii. . .taifa lingine. Sasa, huenda lilionekana la kigeni sana kwa watu, wapitaji walioyaona mawe haya yaliyoonekana ya ajabu yakikatwa. Lakini Mungu, katika njia Yake Mwenyewe, alikuwa akifanya jambo fulani.

43 Nafikiri Yeye anafanya jambo lile lile, leo hii, ku—kuonyesha mfano wa mfano wa kile hilo lilikuwa. Yeye anayakata jinsi apendavyo.

44 Sasa tunaona, ya kwamba hizo nyenzo zinazokatwa katika nchi ya uenyeji wao, zilikuwa ni za kipekee kwa nye—nyenzo zilizokatwa kwenye nchi ya uenyeji wa mtu mwingine. Nasi tunaona kwamba zote zilisafirishwa kutoka, kwa mkokoteni wa maksai, na kadhalika. Na baadhi yake zilikuja kwa bahari, na zingine kwa mkokoteni wa maksai, na zingine zilielea majini zikashuka Jopa kwa chelezo, na kadhalika, kisha zikakokotwa hadi ndani. Kwa jumla, zilikuwa zikija mahali pamoja, kwa kusudi moja, na hilo lilikuwa ni kuitimiza amri ya Mungu.

45 Nayo mierezi ilikatwa huko Lebanoni. Nayo mierezi ya Lebanoni ilikuwa ndiyo mierezi iliyosifika sana ulimwenguni kote. Kama vile siku hizi, kuna mahali pamoja ambapo mti mwekundu unapatikana, hapo ni California. Pia kuna mahali pamoja, wanapaita, huko Afrika, kule Mossel Bend, kuna mti wenye sifa sana kule unaoitwa mti mnuki. Haupatikani mahali pengine popote ila huko. Pia kuna miti mbalimbali inayopatakikana mahali mbalimbali nchini. Nayo mierezi ilipatikana Lebanoni, mwerezi ulio juu sana, mrefu, mgumu, kwa sababu ilikuwa ni nchi yenye joto. Kadiri nchi ilivyo na joto, ndivyo mti unavyozidi kuwa mgumu. Na—na kadiri nchi ilivyo na baridi, ndivyo unavyokuwa mwororo.

46 Hilo lina matumizi ya kiroho, pia. Baridi na kutojali, mwororo na unaelea majini. Lakini ukiwa na joto, umejazwa Roho, unashikana pamoja ukawa na faida mkononi mwa Bwana.

47 Sasa, tunaona ya kwamba mierezi hii mikubwa ilikatwa na wakata miti. Nao walikuwa . . . walikuwa na ramani. Nao wakaileta pamoja kutoka mahali mbalimbali ulimwenguni.

48 Sasa, kama mkiangalia, Sulemani kamwe hakutofautiana hata kidogo na kiolezo ambacho Musa aliona juu ya Mlima Sinai, Mbinguni. Musa, wakati aliporudi kutoka kwenye ono lake, alipiga hema, na kuifanya sawasawa kabisa na yale aliyoona Mbinguni. Basi wakati Sulemani alipolijenga hekalu, yeye alilifanya sawasawa kabisa na vile a—alivyoona kile kielelezo, ule mfano. Musa alipiga hema, kwa ajili ya m—mfano wa milele, kwa sababu ilihamishwa mahali mahali. Lakini, Sulemani, yeye alifanya ma—maskani sawa kabisa na mfano Musa alioona Mbinguni. Yote iliwekwa pamoja, ikawekwa katika utaratibu, sawasawa kabisa.

49 Ni matumizi ya jinsi gani ya kiroho tungeweza kutumia hapa: kwamba haitupasi kamwe kuyaacha Maandiko. Dumu moja kwa moja na hicho kielelezo. Hiyo ndiyo sababu, ninaamini, ya kwamba jinsi kanisa la Kwanza lilivyopangiliwa, hivyo ndivyo Hilo lingine linapaswa kupangiliwa, hivyo ndivyo kila moja linavyopaswa kupangiliwa, jinsi tu lilivyokuwa hapo mwanzo. Nami ninaamini ya kwamba Mungu amelipanga jinsi hiyo, ninaamini, lile Kanisa halisi. Vema.

50 Zile nyenzo, zilikatwa katika nchi ya uenyeji wao, zikaletwa mahali pamoja. Lakini zilipoletwa pamoja . . . Ninasoma sasa kutoka kwenye mlango wa 16, ama kunukuu kutoka kwake. Sasa, zilipoletwa pamoja, ziliumana kikamilifu, hivi kwamba, katika muda wa miaka arobaini iliyotumika kuusimamsha huo mjengo, hapakuwapo na jiwe moja—moja la kukatwa tena. Hapakuwapo na mlio wa msumeno, wala sauti ya nyundo, kwa miaka arobaini. Nena kuhusu uashi, usanifu majengo!

51 Sasa, hiyo ilionyesha, kwamba, tunapofanya lolote, na kulifanya katika kielelezo ambacho Mungu ametuwekea . . .

52 Sasa, mengi ya mawe hayo yalionekana ya kipekee sana. Bali palikuwapo na mahali hekaluni kwa ajili ya kila jiwe la kipekee, la aina yake. Mungu alikuwa na mahali kwa ajili yake.

53 Huduma zetu, ambazo ni mfano mzuri pale, ama mfano wa mfano wake, zinaonyesha ya kwamba, katika upekee wetu, njia yetu ya kuabudu. Hata hivyo, wakati Hekalu, lile Hekalu halisi ambalo tutalifikia baada ya dakika chache, litakapokuja pamoja, kutakuwapo na mahali kwa ajili ya kila mtu anayetenda kipekee. Huenda tukaonekana kidogo ni wa kuchekesha kwa mtu mwingine, na kutenda kigeni kidogo; lakini, kumbukeni, kuna mahali hapo kwa ajili yetu. Mungu analikata Kanisa Lake.

54 Na kila jiwe dogo lilikuwa na mahali lilipoenea kikamilifu. Pia kumbukeni, lilikatiwa, mbali na mahali litakapowekwa pamoja; lakini, lilipoletwa pamoja, hata halikuhitaji

kusuguliwa. Lilikuwa tayari limesuguliwa. Mungu alikuwa amelifanya lipate kuenea mahali pake.

55 Loo, ni mfano wa jinsi gani hapo tunaouona, wa kiroho, jinsi ambavyo kila karama ya Mungu, kila tendo la kipekee la Wakristo waliozaliwa mara ya pili, katika upekee wao, hata hivyo lina mahali pake. Linaea katika ule Mwili. Linaenda mahali pake panapofaa.

56 Na wengi wetu tunge—tungejaribu kusema, "Sasa, hilo si la Mungu," askari mwema, mtakatifu, wa msalaba aliyewekwa wakfu. Nasi tunasema, "Sasa, tulisimama kanisani hivi majuzi usiku, nasi tukasikia jambo *hili-na-lile*. Hilo haliwezi kuwa ni la Mungu." Lakini kama linaambatana na Kielelezo, kama linaendana na Maandiko, huenda likawa ni la kipekee, bali litakuwa na mahali pake. Mnaona? Litaenea moja kwa moja ndani, na hata halitahitaji kusuguliwa ama kupigwa msasa. Litaenda mahali pake, kwa kuwa yule Msanifu Majengo mkuu, Kristo, analiandaa sasa; la kipekee, moja kwa lingine.

57 Sasa tunaona, katika hili jengo hapa chini, mlango unaofuata, kwamba, katika jengo hili, kulikuwa na jiwe moja ambalo kweli lilikuwa ni la kipekee sana kujipumbaza nalo, kwa hiyo wajenzi wakalikataa. Kwa hiyo wakalitupa tu pembeni, kasema, "Hilo jiwe kweli ni la kipekee sana haliwezi kutumika. Hakuna mahali kama hapo."

58 Sasa, kumbukeni, wajenzi ndio waliopaswa kujua tofauti. Yesu alinena habari zake.

59 Lakini, wakaja kugundua, walikuwa wamelijenga jengo hilo likaenda juu sana hata wakalikosa hilo jiwe. Wala hawakujua mahali jiwe hilo lilipokuwa. Huenda walitafuta kwenye meli zote. Huenda walipitia kwenye kila mkokoteni wa maksai. Huenda waliwatuma wajumbe huko Jopa, na huko chini, kasema, "Kuna mzigo mwingine umeingia?" Ama, "Hivi mlipoteza mmoja barabarani? Kuna kasoro fulani. Kamwe hatuwezi kulipata hilo jiwe la mahali hapa." Basi wakati hawakuweza kulipata, mahali pengine popote, walikuja kugundua, lilikuwa moja kwa moja uwanjani. Lilikuwa ndilo jiwe kuu la pembeni ambalo wajenzi walilikataa.

60 Yesu alinena habari zake, na kusema, "Hivi hamjasoma habari za lile jiwe ambalo wajenzi walilikataa? Lilikuwa ndilo jiwe kuu la pembeni, kichwa cha yote, ambalo jengo lote lilitulia juu yake."

61 Nami nafikiri, katika ku—kujenga siku hizi nyumba ya kiroho ambamo Mungu huabudia, nafikiri huko kumekuwa ni kushindwa kukuu siku hizi miongoni mwa wajenzi. Tumekuja pamoja na madhehebu yetu, nasi tumeyaweka katika uaminifu. Tumewapeleka wavulana wetu shuleni, kuwafunza kuzungumza vizuri mbele ya kusanyiko, tukawafundisha saikolojia na historia ya Biblia. Nasi tumefanya kila kitu, na kujenga

mabenchi mazuri, na kujenga minara mirefu sana, na muziki mtamu, na kadhalika, tumejenga. Lakini tunakuta kwamba kuna kasoro. Tumejaribu kulijenga kutoka kwa nyenzo za kujibunia za wanadamu, yale elimu ingeweza kutoa, yale seminari zingeweza kutoa kwake, yale utaalamu. Tumejaribu kulijenga juu ya elimu, juu ya utaalamu, juu ya dhehebu. Na mambo haya yote hayatafanya kazi mradi tu hatujalikubali Jiwe hili la kipekee, Jiwe hili la namna yake.

62 Lakini jengo lilipoanza kutokeza, walitambua ya kwamba shimo lililoachwa, hilo jiwe la kipekee linalienea, kikamilifu.

63 Hapo ni, ambapo, wajenzi wa kiroho siku hizi. Na hiyo ndiyo sababu lile jengo la Bibi-arusi, wa Kristo, haliko tayari kwa ajili ya Bwana-arusi, ni kwa sababu kwamba wajenzi wamelikataa Jiwe Kuu la Pembeni lililowekwa kwenye Siku ya Pentekoste, ambalo ni ubatizo wa Roho Mtakatifu. Mnaona? Imekuwa ni ya kipekee. Watu wanatenda kigeni. Na wao—wao hawaingii katika utaratibu wa saikolojia yetu—yetu, ya elimu yetu, masomo yetu, kanuni zetu za imani. Halienei mle ndani. Nao wakalitupa nje, kwa sababu Hilo lilikuwa ni la kipekee mno, la namna yake kabisa, haliafikiani kabisa na mi—mipangilio ambayo sisi kama wanadamu tulikuwa nayo, mawazo ya kile Kanisa linapaswa kuwa.

64 "Linapaswa kuwa ni kundi la wanachuoni waliostaarabika. Linapaswa kuwa ni kundi la watu waliovalia nadhifu. Linapaswa kuwa ni kundi la kitu fulani, ambapo..." Tumejaribu kulifanya kuwa ni utaratibu wa kielimu, ama kitu fulani ambacho kingezifurahisha hisi zetu tano, kitu ambacho tungeweza kuona, ama kuonja, ama—ama kugusa, ama—ama kitu fulani. Karibu yote imekuwa kupitia kwa kuona. "Waangalie watu wetu wazuri. Uangalie umati wetu ulio bora zaidi mjini. Meya huja kwetu. Ma—maafisa wakuu wa mji wetu, mkuu wa polisi huja kanisani mwetu."

65 Kisha tunaona ya kwamba, inapofikia kwenye mambo halisi, u—ujenzi, yote tuliyo nayo ni udongo wa kujengea tofali na mwamba. Wala mjengo haukuendelea. Waliikataa ile Njia, lile Jiwe ambalo Mungu alikuwa ameliandaa sana kwa ajili Yake. Walilikataa.

66 Sasa, tunaona, loo, katika mlango unaofuata, kwamba wakati wale wajenzi walipoona kwamba walikuwa wamekosea. Hata hivyo, walikuwa na mawe yale mengine yote pale, lakini sababu hawangeweza kuyaunganisha pamoja ilikuwa ni kwamba kulikuwako na shimo lililosalia. Kulikuwa na kasoro fulani.

67 Sasa, tayari tunayo mawe, mawe ambayo Mungu aliyakusudia kimbele. Mnaona? Nasi tunayo, kote kote tangu Efeso hadi Laodikia. Tunangojea tu lile Jiwe la kichwa ambalo

wajenzi walilikataa, tukikungojea Kuja Kwake, lile Jiwe la kufunika. Na wakati . . .

68 Mawe haya makubwa ni maungamo. Sasa, tunajua ya kwamba maungamo ni jiwe. Sasa, ninii . . .

69 Watu wetu Wakatoliki wanasema kwamba wakati ninii . . . "Yesu akizungumza, na Yeye alisema, 'Juu ya mwamba huu, ama jiwe, nitalijenga Kanisa Langu.'" Sasa, kanisa la Kirumi la Ukatoliki linasema, kwamba, "Ilikuwa ni Petro, kwa kuwa yeye alikuwa ni jiwe, mtu mwenyewe, Simoni Petro." Yeye alirudi nyuma, siku chache baadaye. Sasa tunaona, basi, Mprotestanti anasema, kwamba, "Lilikuwa ni Kristo, lile jiwe." Lakini sio kutokukubaliana, bali kama utaangalia tu hayo Maandiko, haikuwa hata mmoja wa hao.

70 Ilikuwa ni maungamo ya Petro na ufunuo ya kwamba Kristo alikukwa ni nani. Kwa kuwa Yeye aliuliza swali, nalo lilikuwa ni swali ambalo lilihusishwa. "Watu husema Mimi Mwana wa Adamu ni nani?"

71 "Wengine walisema, 'Musa, wengine Eliya, na wengine, mwajua, mifupa ya nabii fulani aliyefufuka, ama kitu fulani. Huyo alikuwa ndiye.'"

72 Lakini Yeye alisema, "Ninyi mwasema kwamba Mimi ni nani?" Hilo hapo swali.

Yeye akasema . . . Petro alisema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

73 Akasema, "Heri wewe, Simoni, mwana wa Yona, kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukulisoma kwenye kitabu. Hukulisikia katika seminari. Lakini Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia. Na juu ya mwamba huu, ufunuo wa kiroho wa Neno la Mungu," ambalo Yeye alikuwa ndiye Neno, "nitalijenga Kanisa Langu; na malango ya kuzimu hayatalishinda kamwe."

74 Hilo ndilo Kanisa halisi; si la udongo wa kujengea tofali, na tofali, na jiwe, na kadhalika, ambavyo huharibika. Bali Kanisa halisi limejengwa juu ya ufunuo wa Neno na mapenzi ya Mungu. Nao wamewekwa katika ule Mwili, tangu wakati wa kanisa la Efeso, kote kote hadi Laodikia sasa. Lakini kile . . .

75 Katika siku ambayo Sulemani alipokuwa amelikamilisha lile hekalu . . . Nalo lile jiwe kuu la pembeni, mara wale wajenzi walipolikubali lililokataliwa, basi lile jengo likaanza kwenda juu.

76 Hebu niseme hili kwa uchaji wote na kwa heshima yote kwa kila mtu katika kila kanisa, na wazo la kila mtu. Wakati wajenzi wetu leo hii wanapolikubali lile Lililokataliwa, badala ya kuwasukumia mbali na kuwaita "kundi la watakatifu wanaojibingirisha, wale wa kipekee wanaofanya maungamo," haraka hivyo lile Jengo litakamilika.

77 Lakini je, mlitambua? Lile jengo likiisha kukamilishwa, lingali lilikuwa ni jengo tupu. Hakukuwako na kitu ndani yake ila fenicha. Kwa hiyo Sulemani alikuwa amefanya yote aliyoweza kufanya. Sasa, ile siku kuu ya kuweka wakfu ikawadia, wakati walipokuwa wakitaka kuweka wakfu jengo hili waabuduo wapate kuabudu kitu fulani. Sasa, pasipo na kitu mle cha kuabudu, lile jengo lingalikuwa ni bure. Lakini hilo jengo lilikuwa tayari sasa kwa ajili ya kuwekwa wakfu.

78 Ndipo wakati Walawi na makuhani, pamoja na maelfu ya baragumu zikiipasua anga; huku mwana-kondoo baada ya mwana-kondoo akifa, kwa ajili ya sadaka ya dhambi. Nao Walawi wakachukua mahali pao, wakaenda pembeni na kuchukua boriti zao, wakazichomeka kwenye vipuli vya lile sanduku, ambamo zile mbao za jiwe zilikuwa ndani. Mbao mbili za jiwe; jiwe lile lile. "Hawa wawili ni mmoja," amri ile ile, agano lile lile. Wakati, mbao hizi mbili za jiwe, pamoja na makerubi na mabawa yao yametandazwa, mmoja kwa mwingine. Wakati, Walawi hawa, kundi hilo lililowekwa wakfu ndilo pekee lingaliweza kulibeba lile sanduku. Hakuna mtu angaliweza kuligusa, nje ya hao; kama angaliligusa, alikufa. Nao wakazichukua boriti hizi, wakijua ya kwamba waliwekwa wakfu kutumikia kitu hiki chenyewe. Nao wakazichomeka hizo boriti kwenye vile vipuli, kama walivyoagizwa (Musa alivyokuwa ameagizwa) na Mungu, kujenga mjengo wa lile sanduku.

79 Nao wakalichukua, kutoka hemani mwake. Wakaanza kwenda taratibu; huku baragumu ikilia, zeze zikicheza, moshi ukipanda juu kutoka kwa wanyama waliokufa waliokuwa wakitolewa dhabihu mbele za Yehova. Wakashuka kupitia hilo jengo la kuwekwa wakfu, mpaka wakalileta kwenye mahali pake pa kutulia, ambapo liliingia vizuri kwenye matundu ya mahali hapo pakubwa palipoandaliwa kwa ajili yake. Ndipo wakati lilipoingia vizuri, na hatimaye likafikia mahali pake pa kutulia, lile sanduku, Biblia ilisema, kwamba, "Bwana alishuka mahali hapo, mpaka akalijaza hekalu lote. Nguzo ya Moto ikashuka mle ndani pamoja na utukufu mkuu sana wa Mungu hata wahudumu wasingeweza kuhudumu tena, kwa sababu ya utukufu wa Mungu."

80 Hapo ndipo hatimaye lilipopata mahali pake pa kutulia, ule utukufu wa Shekina uliowafuata hao; jiwe la kufunika, sio la pembeni; jiwe la kufunika, kitu muhimu. Mawe mengine yote hayakuwa na faida yoyote kufikia wakati huo. Lakini hili jiwe kuu likaingia, jiwe la kichwa, na kupachukua mahali pake kwa ajili ya mahali pa kupumzikia, kwa ajili ya kizazi hicho. Utukufu wa Mungu ulipajaza mahali hapo ambapo walikuwa wameketi, na kulikuwako na utukufu wa Shekina juu ya jengo hilo lote. Nao huo utukufu ulikuwa ni mkuu sana hata makuhani wasingeweza kuhudumu kwa sababu ya huo utukufu.

81 Sasa, tunasoma sasa, na kuchukua kutoka kwenye kule kuwekwa wakfu kwa hekalu. Hebu twendeni sasa kwenye Matendo mlango wa 7 tena, na kifungu cha 44, nasi tuanzie kwenye nukuu. Stefano, katika mahubiri yake yaliyotambulikana wakati akihubiri, yeye alisema, "Sulemani alimjengea Yeye hekalu, kwa sababu iliahidiwa kupitia Daudi ya kwamba yeye angeninii..." Mungu alimwahidi Daudi ya kwamba yeye angelijenga hekalu. Naye Mungu...

82 Katika mfano, ambao ulikuwa uondolewe na mfano wa mfano, kama vile tu dhabihu ya wana-kondoo kwenye kule kuweka wakfu ilivyokuwa ni mfano wa yule Mwana-kondoo halisi akija kwa ajili ya dhabihu. Mambo yote ya kawaida yakiwa ni mfano wa ya kiroho.

83 Nasi tunaona ya kwamba, wakati hili lilipotukia, Stefano ananena habari zake. Yeye alisema, "Baba zetu walipata fadhili mbele za Mungu, naye Sulemani akamjengea hekalu. Lakini, ila, Yeye aliye Juu hakai kwenye mahekalu yaliyofanywa kwa mikono. Kama nabii alivyosema, '"Mbingu ni Kiti Changu cha Enzi, na nchi ni pa kuwekea miguu Yangu, basi iko wapi nyumba ambayo mngeweza kunijengea Mimi? Mbingu ni Kiti Changu cha Enzi, nchi ni mahali pa kuwekea miguu Yangu, basi mngewezaje kunijengea Mimi nyumba ya kukaa ndani?"'"

84 Ndipo, jinsi Waebrania 10:5 ilivyo nzuri, "Lakini Mwili umeniwekea tayari," ikionyesha ya kwamba Mungu alikuwa anaenda kuishi katika Mwili. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] "...umeniwekea tayari." Loo! Basi wakati mwili huu ulipokuwa umefanywa dhabihu, Mwana-kondoo anayefaa alipokuwa ametolewa dhabihu, basi kulikuwa kunakuja, Mungu alikuja kwenye Mwili Wake Mwenyewe, ambao ulikuwa ni Bibi-arusi Wake.

85 Napo palikuwapo na mahekalu mia moja na ishirini ambayo Mungu alikuwa ameumba, yaliyokuwa tayari kwa ajili ya kuweka wakfu, ambayo yalikuwa yameondolea mbali kutokuamini kwao kwote kutoka kwayo. Nayo yalikusanyika katika chumba cha juu, yakangojea siku kumi, kwa ajili ya ibada ya kuwekwa wakfu. Ndipo wakati yalipokuwa yamejisalimisha kikamilifu, Mungu alishuka chini tena katika utukufu wa Shekina, na kuijaza nyumba yote yalimokuwa yameketi. Mungu alifanya nini? Kama vile lile sanduku likiangukia matundu yake halisi kwa ajili ya ujumbe wa siku hizo, Mungu alishuka katika mkondo Wake mzuri; sio katika dhehebu ama katika jengo lililofanywa kwa mikono, bali ndani ya moyo wa wanadamu. Yeye alishuka mahali Pake, kwa ajili ya siku za mwisho, ambazo alisema nabii Yoeli. "Itakuwa katika siku za mwisho, nitaimwaga Shekina Yangu juu ya wote wenye mwili. Wana na binti zenu watatabiri. Vijana wenu wataota ndoto. Wazee wataona maono." Mungu akaja kwenye mahali Pake pa

kupumzikia, ambapo anapata raha. Sio katika jengo, bali katika moyo wa watu Wake, Yeye hupata raha.

86 Ni aibu ya jinsi gani, ni fedheha jinsi gani, ni maangamizi jinsi gani ambayo ufanisi wa kijibunia wa Nimrodi ulifikia wakati huo! Wakati Nimrodi alipojaribu kujenga m—mjengo ama dhehebu ambalo lingefika juu mbinguni, Mungu alilivuruga. Ikawa ni aibu, badala ya kuwasaidia watu. Yeye aliivuruga lugha ya wanadamu. Mmoja asingeweza kuzungumza na mwenziwe. Ilivunja udugu.

87 Lakini wakati Mungu alipokuja kwenye hekalu Lake Mwenyewe, Kanisa, wa—wale watu, wakati alipowajia, Yeye alilijaza Hilo, yale mahekalu yaliyokuwa yamewekwa wakfu.

88 Kama tu Yeye alivyofanya kwenye hekalu la Sulemani. Alilijaza, sio kwa kanuni za imani, sio kwa madhehebu, bali kwa nafsi Yake. Yeye alilijaza hekalu kwa utukufu Wake wa Shekina.

89 Ndivyo alivyofanya kwenye Siku ya Pentekoste. Yeye aliyajaza hayo mahekalu mia na ishirini yaliyokuwa huko juu, kwa nafsi Yake, kwa Roho Mtakatifu Mwenyewe. Ule utukufu wa Shekina ukawafungukia. Ndipo basi yale Nimrodi aliyoshindwa kufanya, kujenga hekalu ambamo kila mtu alinena kinyume na yale angeweza kuelewa; Mungu alishuka, na kwa lugha moja ya Kigalilaya, akamfanya kila mtu kufahamu yale Yeye aliyokuwa akisema, nao wanajua ililetwa. Huyo hapo Mungu katika hekalu Lake. Mungu kwa hekalu Lake lililowekwa wakfu, sio kwa mafanikio ya kujibunia ya mwanadamu, sio kwa yale mwanadamu aliyofanya; bali yale Mungu aliyofanya Mwenyewe.

90 Loo, ni upumbavu, kwa hao watu. Hawalipati. Walizaliwa wasilipate, kwa hiyo hawatalipata. Biblia inasema hivyo. Vema.

91 Mungu daima hulijaza hekalu Lake. Kwenye siku ya kuweka wakfu Yeye hulijaza hekalu Lake. Yeye hulijaza kwa nafsi Yake. Jambo lile lile, leo hii. Mungu atalijaza kila hekalu ambalo litajiweka wakfu kikamilifu Kwake, watu wowote watakaojiweka wakfu. Hekalu si hili jengo dogo hapa. Hekalu si lile lililoko Salt Lake City. Hekalu si lile lililoko Urumi. Hekalu ni wewe. Wewe ndiwe hekalu ambalo Mungu anataka kuishi ndani yake na kujidhihirisha Mwenyewe kupitia kwake, ili mataifa yote yaweze kumjua Yeye. Ninyi ni sura zilizo hai za Mungu, ambazo Mungu anataka kufanya kazi kupitia. Na wakati wowote ambapo mwanamume yeyote ama mwanamke yeyote atasahau uongo wote ambao wamesikia ulimwenguni, na kurudi kwenye mstari wa Maandiko, na watakaa mstarini.

92 Kama tu, Sulemani alivyofanya kwa yale Musa aliyofanya. Musa alivyofanya kwa yale Mungu aliyofanya. Mungu daima aliyaheshimu.

93 Na kama tutarudi kwenye kule kuwekwa wakfu asilia na tutaifungua mioyo yetu na kujifanya tupu, Mungu, katika

kuweka wakfu, tunapompa Yeye, atalijaza hekalu letu kwa utukufu Wake wa Shekina. Ndipo Mungu aliye hai atakuwa akitenda kazi katika Kanisa lililo hai, miongoni mwa watu walio hai, na atausambaza utukufu Wake. Ndipo, pamoja, siku moja, mmoja akiwa *hivi*, na mmoja *hivi*, na mmoja sehemu moja ya nchi, watakusanyika kumfanyiza Bibi-arusi. Tutanyakuliwa hewani, kumlaki Yeye.

94 Sasa, kanisa hili la kupendeza, jengo hili ambalo watu, kwa ishara zao za maisha yao, pamoja na upendo wao kwa Kristo, waabuduo wanaweka wakfu, leo hii, mahali hapa pa kuabudia, ambapo watu wangeweza kuja na kuabudu. Sasa, ombi langu aminifu ni kwamba kila ibada itaninii . . . mwabuduo ataweka wakfu hekalu lake mwenyewe, kuabudu, katika hekalu linalowekwa wakfu kwa ajili ya ibada. Huko ndiko kuwekwa wakfu halisi.

95 Kwa hiyo kwa kuwa muda wetu umekwisha, ila Mungu hana wakati. Hebu tukumbukeni. Imechelewa jinsi gani? Ninawaangalia wazee. Huenda ikawa muda umeenda kuliko mnavyodhania. Ninawaangalia vijana, wasichana wadogo.

96 Tazameni, maskini watoto hawa wadogo walipatikana, wamekatakatwa, hivi majuzi, hao wasichana wadogo wamebakwa. Ni wangapi wao wanaokufa kila mwaka? Maelfu, kwa mishtuko ya moyo, kansa, polio, chochote kinachoweza kuwaua, ajali barabarani.

97 Hatujui, ni vijana kiasi gani ama ni wazee kiasi gani, wakati huo utakuja lini? Kadi yako itaitwa lini kutoka kwenye rafu? Hakuna ajuaye hilo ila Mungu. Hiyo ni kweli.

98 Kwa hiyo wakati ungali hapa, leo hii, katika kuweka wakfu kwa nyenzo hii hapa, ambamo waabuduo wanakuja kumwabudu Mungu aliye hai, mbona tusijiweke wakfu sisi wenyewe kwa ibada ya Mungu aliye hai, na kumwacha Yeye atujaze kwa nafsi Yake? Ndipo basi tutauona utukufu wa Shekina ukirudi tena kwenye nyumba ya Mungu aliye hai, ambayo ni mwili wa mwanadamu, Kanisa la Mungu aliye hai, pamoja, katika uamsho mkubwa ambao ungeenea kote humu nchini, kuizunguka miji hii, na kote kupitia hapa. Kutakuwako na kelele nyingi sana. Mbona, wa—wasingeweza kuzikomesha. Hakuna njia ya kufanya hivyo.

99 Unafikiri ungalimkomesha Stefano? Mbona, yeye alikuwa kama nyu—nyumba inayowaka moto katika upepo mkali. Mbona, usingeweza kumkomesha. Hata lile Baraza la Wazee lisingeweza kumkomesha. Pia, mwajua, hata mauti yenyewe hayakumkomesha. Yeye aliendelea kuishi. Na angali anaishi leo hii. Naye daima ataishi, kwa sababu yeye alikuwa na Uzima wa Milele, na nyumba iliyowekwa wakfu kwa utumishi wa Mungu.

100 Nafikiri jambo la kanisa hili kufanya, asubuhi ya leo, kwa minajili ya yote ambayo yamefanywa: wakati tukimkabidhi

Mungu hili jengo, kwa ajili ya ibada, hebu tujitolee wenyewe, pia.

Hebu tusimame kwa dakika moja tu sasa.

101 Kila mmoja katika njia yako mwenyewe, kulingana na njia unayotaka kuomba. Ninajiweka wakfu tena leo, mimbarani, kwa utumishi wa Mungu. Ninamtaka kila mmoja wenu afanye hivyo. Tunapoliweka jengo hili wakfu kwa Mungu, hebu tujiweke wakfu.

102 Baba yetu wa Mbinguni, tumekusanyika hapa kwa unyenyekevu na uaminifu sana asubuhi ya leo, katika shukrani kubwa kwa ajili ya upendo ambao Wewe umelionyesha kusanyiko hili, kwa kuwapa jengo hili kwa ajili ya ibada, na kwa kulipa kusanyiko hili mchungaji huyu, mhudumu wa Neno.

103 Na sasa, Baba wa Mbinguni, kama mahali panapowekwa wakfu kwa ajili ya ibada, sisi kama waabuduo tunaweka kando kila kitu, kila kutokuamini, kila wazo lisilo jema, kila kitu kisicho kama Wewe, na kila kitu ambacho kingetenda ndani yetu kinyume na Neno Lako; chochote, kanuni yoyote ya imani, wazo lolote la kimadhehebu, ama wazo lolote ambalo jirani ama mtu yeyote mwingine, hapa na pale pia, ama popote linapoweza kuwa, ambalo lingetujia kama wazo la mtu huyu, ingawa ameaga dunia, ingawa ni chombo kitakatifu, kilichotakaswa; chochote kile, mtu yeyote, ama Malaika, ama mwenye uhai, ama ufunuo, ama chochote kiwezacho kuwa ambacho ni kinyume na mpango Wako kwa ajili ya siku hizi zilizonenwa katika Neno Lako. Si yale mtu fulani aliyosema; bali yale Wewe uliyosema! Kwa kuwa imeandikwa, "Neno la kila mtu na liwe uongo, na Langu kweli." Iwapo kuna lolote ndani yetu ambalo lingetuzuia tusiliamini Neno la kweli, na kuujua ufunuo wa Kristo, kama Yeye alivyomwambia Petro, "Juu ya mwamba huu, ninalijenga Kanisa Langu." Iwapo kuna lolote kinyume na hilo, liondoe kwetu, Bwana. Tunaliweka kando, sisi wenyewe. Tunalitupa nje. Na kukubali mahali pake, lile Jiwe Kuu la Pembeni, yule Roho Mtakatifu ambaye ndiye msingi wa Kanisa halisi la Mungu. Tunakubali hilo.

104 Baba, libariki kanisa hili dogo. Idumishe hii mijengo juu, na ujalie waabuduo wakusanyike hapa, wakati baada ya wakati, kila ibada. Jalia kuwe na upendo mkubwa sana wa Mungu miongoni mwao, hata hawawezi kutengana mmoja na mwingine, mioyo yao inatamani kuja pamoja, kwenye nyumba ya Mungu. Tujalie, Bwana.

105 Pia jalia wakolee chumvi sana, kama vile Wewe ulivyosema, "Ninyi ni chumvi ya dunia." Jalia maisha yao yakolee sana na kukamilika katika Roho Mtakatifu, mpaka jamii yote jirani itatamani kuwa kama wao. Tujalie, Bwana. Wafanye mifano. Tujalie, Baba.

106 Sasa, chukua kila mmoja wetu, wakati tukilikabidhi hili kanisa, hili jengo, Kwako. Tunajitolea Kwako, katika kujiweka wakfu kwa uchaji. Pia jalia Roho Mtakatifu katika Nguvu Zake zote za Kiungu, katika utukufu Wake wa Shekina, aje akibingirika chini kupitia umilele, aingie mioyoni mwetu, Bwana, apate makao Yake kwa ajili ya siku hizi za mwisho. Nawe utuite kwenye huduma, kama wajumbe, labda si kwa ajili ya mimbara, bali kwenye kituo cha petroli, kwenye beseni ya kuoshea, popote pale, kumshuhudia mwuza maziwa, mvulana wa magazeti, ama yeyote yule. Tufanye shuhuda na mawe yaliyo hai yaliyojaa utukufu wa Shekina, Roho Mtakatifu, Mwenyewe. Ijaze mioyo na maisha yetu, Baba.

107 Ndipo wakati ibada zote zimekwisha, hapa duniani, tujalie kikamilifu, huku tumekatwa katika njia zetu wenyewe ambazo Mungu ametufanya, tukusanyike pamoja katika lile Kanisa kuu, linaloitwa Bibi-arusi. Yeye atanyakuliwa kutoka kwenye maskani hii ya kukaliwa hapa, na Yeye atabadilishwa katika dakika moja, kufumba na kufumbua jicho. Naye atanyakuliwa pamoja na Yeye, kumlaki Yeye hewani, kwenye ile Karamu ya Arusi ya Mwana-kondoo. Kwa kuwa tunajitoa wenyewe, na kanisa hili, watakatifu na waliowekwa wakfu tuwezavyo, Baba, kwa utumishi Wako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mwaweza kuketi.

108 Ni wangapi wenu wanaosema, "Kwa neema ya Mungu, na pamoja na msaada wa Mungu, ninasalimisha moyo wangu. Njoo, Bwana Yesu, na unijaze tu kwa wema Wako. Nifanye tu kile unachotaka niwe. Ikiwa niko kinyume, na katika kujiliwa ambako Wewe umeniweka, kule kutenda kazi, ambapo nina haki ya kutoa *hivi* ama *vile*, usiniache niwe jiwe lililokatwa vibaya, bali jalia nijitolee kwa msumeno unaonifanya kile nilicho, kile Wewe unachotaka niwe"? Hivyo ndivyo tunavyolitaka, sivyo?

109 Na tuinue tu mikono yetu sasa na kuimba wimbo huu adhimu wa kale wa kanisa, ninapoirudisha ibada yenu kwa mchungaji wenu.

> Nampenda, nampenda
> Kwani alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

110 Sasa hebu tuuvumishe. Sasa peana mikono na mtu fulani aliye karibu nawe, useme, "Mungu akubariki, ndugu, jiwe Kanisani." Na Mungu akubariki, ndugu, mawe katika Kanisa. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu. Mungu akubariki. Mungu akubariki, ndugu.

> . . . Alinipenda kwanza
> Na kununua wokovu wangu
> Mtini Kalvari.

111 Sasa na tuyafunge macho yetu, tuinamishe kichwa chetu, na kuinua mikono yote miwili juu Kwake.

Nampenda, nampenda
Kwani alinipenda kwanza . . .

62-1111M Kuweka Wakfu
Full Gospel Apostolic Church
Elizabethtown, Kentucky Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

## Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.


Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:


Voice Of God Recordings

P.O. Box 950, Jeffersonville, Indiana 47131 U.S.A.

www.branham.org